

HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKURUGENZI MTENDAJI,
Simu: +255 (027) 25 39 603/2
Nukushi: +255 (027) 25 39 603,
Barua pepe: ded@longidc.go.tz



S. L. P 84,
LONGIDO.

Kumb. Na. HW/LONG/VOLI/U/02/117

26 Septemba, 2024

Ndugu, Wananchi Wote,
Halmashauri ya Wilaya ya Longido,
LONGIDO

MAELEKEZO YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA KWA WANANCHI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO.

Maelekezo haya yanatolewa kwa mujibu wa Kanuni Na.9 ya Tangazo la Serikali Na.571 la tarehe 12/07/2024.


Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido anawaelekeza Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido kwamba:-

1. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utafanyika tarehe **27/11/2024**;
2. Uandikishaji wa wapiga kura utafanyika kuanzia tarehe **11** hadi **20/10/2024** kwa muda wa siku kumi (10);
3. Wapiga kura wataandikishwa katika vitongoji vyao kuanzia saa **2:00 asubuhi** hadi **saa 12:00 Jioni**;
4. Uchaguzi utafanyika katika ngazi za vijiji na vitongoji kuanzia saa **2:00 asubuhi** hadi saa **10:00 Jioni**;
5. Wananchi wote mnatakiwa kujandikisha na kujitokeza siku ya kupiga kura kwa ajili ya uchaguzi huu;
6. Wananchi wote wenye umri wa **miaka 21** na kuendelea mnakaribishwa kuchukua fomu za kugombea nafasi mbalimbali za uongozi

(Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, Mjumbe wa Serikali ya Kijiji na Mjumbe wa Viti Maalumu) katika Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

7. Viongozi waliopo madarakani watakoma kuwa viongozi mnamo tarehe **25/10/2024** ili kupisha mchakato wa uchaguzi kuendelea;
8. Fomu za wagombea nafasi za uongozi zitapatikana katika Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuanzia tarehe **01/11/2024** na tarehe ya mwisho ya kurejesha fomu hizo itakuwa ni tarehe **07/11/2024** saa **10:00 Jioni**;
9. Uteuzi wa wagombea utafanyika tarehe **08/11/2024** na fomu za wagombea zitabandikwa katika Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
10. Muda wa kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi wa wagombea utakuwa ni tarehe **08 hadi 09/11/2024**;
11. Uamuza dhidi ya mapingamizi yote ya uteuzi wa wagombea utakuwa ni tarehe **08 hadi 10/11/2024**;
12. Muda wa kukata rufaa dhidi ya uamuza kuhusu pingamizi utakuwa ni tarehe **10 hadi 13/11/2024**.
13. Uamuza wa kamati ya rufaa utakuwa ni tarehe **10 hadi 13/11/2024**;
14. Kampeni za uchaguzi zitaanza tarehe **20 hadi 26/11/2024**; na
15. Mtu yeoyote atakuwa ametenda kosa la Kiuchaguzi endapo:-
 - i. ataharibu Orodha ya Wapiga Kura au nyaraka zozote zinazohusiana na uchaguzi;
 - ii. atatoa taarifa za uongo ili aweze kupiga kura au kuchaguliwa kuwa kiongozi;
 - iii. atajandikisha au kupiga kura zaidi ya mara moja;
 - iv. atawatishia wapiga kura au wagombea ili kuharibu uchaguzi; na
 - v. endapo atatangaza matokeo ya uchaguzi kabla hayajatangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo;

Serikali za Mitaa Sauti ya Wananchi Jitokeze Kushiriki Uchaguzi.



Nassoro B. Shemzigwa

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO.**

